**Best Start Kindergarten Assessment**
**Information for parents and carers**

# Tathmini Bora ya Kuanza kwa Chekechea

## Taarifa kwa wazazi na walezi

Wazazi na walezi wapendwa,

Tathmini Bora ya kuanza kwa chekechea itafanyika shuleni kwetu katika Muhula wa 1.

Tathmini Bora ya Kuanza kwa Chekechea ni tathmini ya nchi nzima ambayo husaidia kuwaonyesha walimu ujuzi wa kusoma kuandika na kuhesabu wa kila mwanafunzi mwanzoni mwa shule ya chekechea. Hii huwasaidia walimu kupanga masomo ili kusaidia vyema mahitaji ya kila mtoto ya kujifunza.

Watoto huja shuleni wakiwa na uzoefu, ujuzi na uwezo mbalimbali. Wengine wanafahamu vitabu, wanaweza kutambua herufi za alfabeti au hata kuandika majina yao au kuhesabu hadi kumi, wakati wengine bado hawajajifunza ujuzi huu.

Tathmini Bora ya Kuanza kwa Chekechea huwapa walimu fursa ya kuketi na mtoto mmoja mmoja, wakizingatia kile ambacho mtoto anaweza kufanya.

Tathmini si mtihani lakini huwapa walimu taarifa muhimu ili kusaidia ujifunzaji wa mtoto wako shuleni. Iwapo ungependa kumtoa mtoto wako shuleni asishiriki katika tathmini, tafadhali wasiliana na sule.

Kartasi ya maelezo iliyoambatishwa hutoa habari zaidi juu ya Tathmini Bora ya Kuanza kwa Chekechea.

Tafadhali wasiliana na shule ikiwa una maswala kuhusu Tathmini Bora ya Kuanza kwa chekechea

## Huduma ya Ukalimani wa Simu

Iwapo unahitaji mkalimani ili kukusaidia kuwasiliana na shule, tafadhali pigia Huduma ya Ukalimani wa Simu kwa nambari 131 450 na uombe mkalimani katika lugha yako. Mkalimani atapiga simu shuleni na atakaa kwenye laini kusaidia mazungumzo. Hautatozwa kwa huduma hii.

Mkuu wa shule